

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



Kumb. Na.DCC/C.M/3

01 Juni, 2024

**TANGAZO LA AJIRA YA MUDA**

Mkurugezi wa JIJI Dar es Salaam anawatangazia Watanzania wote wenye sifa nafasi ya kazi ya kukusanya ushuru wa Soko.

**I. WAKUSANYA USHURU WA SOKO  
(NAFASI - 50)**

**SIFA ZINAZOHITAJIKA**

1. Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne
2. Awe na elimu ya Cheti/ Stashahada ya Uhasibu au Uongozi wa Biashara kutoka Chuo/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.

**KAZI/MAJUKUMU**

1. Kukusanya ushuru wa Soko
2. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wake.

**MASHARTI KWA UJUMLA:**

1. Mwombaji lazima awe Raia wa Tanzania.
2. Awe amehitimu na kupata cheti cha kidato cha Nne  
NB:"Results Slip" hazitakubadilika.
3. Awe na cheti cha kuzaliwa.
4. Awe na umri kati ya miaka 18-45.
5. Ajira ni ya mkataba wa miezi sita [6].

6. Mwajiri atalipa mshahara wa Tsh.7,000 kwa siku yenye kuleta jumla ya 210,000/= kwa mwezi.

**Barua zote ziambatane na nyaraka zifuatazo:**

- (i) Nakala za vyeti vya mwombaji vilivyothibitishwa ambayo ni:
- Cheti cha kidato cha nne
  - Cheti cha Taaluma
  - Cheti cha Kuzaliwa.
  - Kitambulisho cha Taifa
- (ii) Picha ndogo ya rangi (colored Passport size moja ya hivi karibuni).
- (iii) Waombaji wenye sifa pungufu au zaidi na zilizotajwa hapo juu hawaruhusiwi kuomba kwani maombi yao hayatafanyiwa kazi.

Barua ambazo hazikuambatanishwa na nyaraka zilizotajwa hapo juu hazitashughulikiwa.


**JINSI YA KUTUMA MAOMBI:**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji pamoja na namba ya simu zitumwe kwa anuani ifuatayo hapa chini;

**MKURUGENZI WA JIJI  
HALMASHAURI YA JIJI  
S.L.P. 20950  
DAR ES SALAAM.**

Mwisho kupokea maombi ni tarehe 14/06/2024 saa 9.30  
Mchana

Imetolewa na:

  
Tabu P. Shaibu

**KAIMU MKURUGENZI WA JIJI**

2